



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA**



**MKOA WA GEITA:**

S.L.P. 139,  
**GEITA.**

Tafadhali unapojibu taja:  
**Kumb. Na. GDC/L.20 /22/99**

**18/12/2023**

**TANZANIA INVESTMENT CENTER,**  
**ZONAL MANAGER,**  
**S.L.P 638,**  
**MWANZA.**

**YAH: UTHIBITISHO WA UMILIKI WA VIWANJA ENEO LA KATA YA**  
**RWAMGASA, KIJJI CHA KILOMBERO I NA KILOMBERO 2,**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA**

Tafadhali rejea kichwa cha habari hapo juu,

2. Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita inapenda kuthibitisha kuwa Kampuni ya **JIUDING MINING INVESTMENT COMPANY LIMITED** imenunua kihalali eneo lenye ukubwa wa Ekari **15** lililopo Kitongoji cha Iseni, kijiji cha Kilombelo I na eneo la Ekari 10.6 lililopo katika kitongoji cha Ibisabageni, Kijiji cha Kilombero 2 - kata ya Rwamgasa katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita, wameuziwa na wananchi wa Rwamgasa kupitia serikali za vijiji, maeneo hayo yana leseni za uchimbaji na utafiti wa madini. Hivyo ni maeneo yao halali.

3. Kampuni ya Jiuding imeanza shughuli ya uchenjuaji wa Madini ya Dhahabu toka mwaka 2021 kwenye eneo lenye ukubwa wa Ekari 10, Ukaguzi wa Mazingira umekuwa unafanyika mara kwa mara hii ni kutokana na kwamba mradi ukiwa unataka kuanza kutekelezwa au ukiwa unaendelea kutekelezwa lazima kaguzi mbalimbali za Mazingira zifanyike, Ofisi ya Mkurugenzi iliwashauri wawekezaji kupanua /kuongeza eneo la uzalishaji ili waweze kuendesha shughuli zao kwa ufanisi bila kuathiri Mazingira.

4. Kampuni imefanya jitihada za kuongeza eneo la uzalishaji kupitia serikali ya kijiji, ambapo imefanikiwa kupata Ekari 15 kutoka kwa wananchi ambao wameridhia kutwaliwa kwa maeneo yao ili kupisha kampuni kuendelea na kazi pia wamenunua

eneo la Ekari 10.6 katika kijiji cha Kilombero 2 ndani ya leseni yao ya utafiti, wananchi wote wamelipwa fedha zao na hakuna mgogoro wowote.

4. Kwa barua hii, nawaleta kwako wawekezaji hawa **JIUDING MINING INVESTMENT COMPANY LIMITED** ili uendelee na utaratibu mwingine kama inavyotakiwa kulingana na Sheria ya Uwekezaji lengo likiwa ni kuwavutia wawekezaji ili waendelee na shughuli zao za uzalishaji na kuongeza uchumi wa nchi kupitia kodi ya Huduma na tozo mbalimbali za nchi.

5. Mihtasari ya vijiji, coordinates na mikataba ya mauziano ya mashamba imeambathishwa wa ajili ya ufafanuzi zaidi.

Nashukuru kwa ushirikiano wako.



Karia R. Magaro  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
HALMASHAURI YA WILAYA GEITA

**Nakala:-**

Mkurugenzi Mtendaji,  
JIUDING MINING INVESTMENT CO. LTD,  
S.L.P 223,  
**GEITA.**

**- Kwa taarifa.**

Baraza la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC),  
Ofisi za kanda ya ziwa Victoria,  
S.L.P 11045,  
**MWANZA.**

Afisa Mtendaji,  
Kata ya Rwamgasa,  
Halmashauri ya Wilaya ya Geita,  
S.L.P 139,  
**GEITA.**

**- Kwa taarifa.**

Barua pepe: [ded@geitadc.go.tz](mailto:ded@geitadc.go.tz), Simu Na.: 028-25200610, Nukushi Na.: 028-2520003